**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

**UKUMBI WA MIKUTANO WA JAKAYA KIKWETE, DODOMA**

**5 JUNI, 2026**

- ***Mhe. Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***
- ***Mhe. Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, Waziri wa Nchi – Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), na Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote mliopo;***
- ***Mhe. Rosemary Sitaki Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa ya Jirani mliopo;***
- ***Dkt. Asha- Rose Migiro, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi;***
- ***Alhaji Adam Kimbisa, Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Dodoma;***
- ***Waheshimiwa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu mliopo;***
- ***Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;***
- ***Mheshimiwa Alimwoni Chaula- Meya wa Jiji la Dodoma;***
- ***Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa, wakiongozwa na Bw. Shigeki Komatsubara, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP);***
- ***Waheshimiwa Wabunge;***
- ***Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya mliopo;***
- ***Viongozi wa Dini;***
- ***Wanahabari;***
- ***Wananchi wa Dodoma na Mikoa jirani;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Kazi na Utu**…………

Awali ya yote napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo, tunapoungana na Jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Mazingira duniani. Nawashukuru waandaaji wa tukio hili kwa kumwalika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mgeni Rasmi katika maadhimisho haya. Kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Rais yuko kwenye ziara ya Kikazi nchini Urusi, hivyo amenituma kumwakilisha. Vilevile, ninawashukuru ninyi nyote mliopo katika ukumbi huu, wakaazi wa Jiji la Dodoma na wananchi wote kwa ujumla kwa kutenga muda wenu kuungana nasi katika maadhimisho haya ya Siku ya Mazingira Duniani.

Hii ni siku pekee katika mwaka ambapo Jumuiya ya Kimataifa imeiweka ili kutambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu na kukumbushana wajibu wetu katika kulinda na kuhifadhi mazingira. Ninafahamu kuwa maadhimisho ya mwaka huu yamehusisha shughuli mbalimbali za kielelezo, zilizotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini, kwa lengo la kutoa elimu ya mazingira kwa umma na kuhamasisha matumizi adili ya rasilimali za mazingira, kwa ajili ya vizazi vya sasa na vijavyo. Ni matumaini yangu kuwa elimu iliyotolewa na shughuli zote zilizotekelezwa katika kipindi hiki cha maadhimisho vitaendelezwa na kuwa sehemu ya maisha yetu ya kila siku.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi na Wadau wa Mazingira;***
Mazingira yana mchango mkubwa sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa pamoja na ustawi wa watu wake. Pale ambapo mazingira yametunzwa vema, basi uchumi na ustawi wa maisha ya watu pia huimarika. Aidha, mazingira ni muhimu katika kuhimili ongezeko la watu duniani. Mathalan, Tanzania inakadirikwa kuwa na watu zaidi ya milioni 67 ambapo ifikapo mwaka 2050, idadi hiyo inakadiriwa kufikia zaidi ya watu milioni 118 (Sensa ya Watu na Makazi, 2022). Ongezeko hilo kubwa litahitaji uwepo wa rasilimali nyingi muhimu zinazotegemea mazingira kama vile maji; chakula; ardhi yenye rutuba inayofaa kwa kilimo; makazi, nishati, mifumo ya huduma za jamii kama vile elimu, afya na usafirishaji. Kwa kutambua umuhimu huo, Dira ya 2050 imejumuisha masuala ya mazingira na ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kama sehemu ya safari yetu ya maendeleo ya kufikia uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu ifikapo 2050.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi na Wadau wa Mazingira;***
Maadhimsho ya Siku ya Mazingira Duniani kama jukwaa muhimu la kitaifa na kimataifa litukumbushe wajibu wetu wa kuunganisha nguvu katika jitihada za kuhifadhi mazingira, na kuhakikisha matumizi adili ya rasilimali nyingi ambazo nchi yetu imejaliwa. Baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatia katika uhifadhi wa mazingira ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira na umuhimu wake; na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa taka hususan katika mamlaka za serikali za mitaa kwa dhana ya uchumi rejeshi, kwa kuwa maeneo mengi bado hali ya usafi haridhishi. Hili linaenda sambamba na kubadili mtazamo wetu wa kuziona taka kama fursa ya kiuchumi na kuzitumia kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vile mbolea, chakula cha mifugo na bidhaa nyinginezo.

Hali kadhalika, kuendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia ambapo hadi sasa, taarifa zinaonesha kuwa matumizi hayo yameendelea kuimarika kutoka 6.9% mwaka 2021 hadi kufikia 28.6% mwaka 2025. Hii ni hatua

nzuri kuelekea lengo tulilojiwekea la Watanzania zaidi ya 80% kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Pia, kutekeleza mikakati mbalimbali ya kisekta ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa kujenga uchumi imara wenye uzalishaji mdogo wa gesijoto, na ulio stahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Katika hili, nafahamu kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa Mpango wa Taifa wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi ambao umeweka misingi ya uhimilivu wa jamii, mifumo ikolojia na sekta za ukuaji wa uchumi dhidi ya athari za mabadiliko ya Tabianchi.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi na Wadau wa Mazingira;***
Jitihada nyingine muhimu ni kuongeza mapato ya ndani yanatokana na fursa za fedha za mabadiliko ya tabianchi zitokanazo na biashara ya kaboni; Mifuko ya Kimataifa ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi; pamoja na ushirikiano wa kikanda na uwili wenye malengo ya kuunga mkono juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Vilevile, uhifadhi wa ardhioevu nchini, ambayo ndiyo chanzo cha mito mingi na ardhi yenye rutuba inayowezesha shughuli za uzalishaji katika kilimo, mifugo, na uzalishaji wa umeme.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi na Wadau wa Mazingira;***
Kwa namna ya pekee, ninaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa afua mbalimbali za uhifadhi wa mazingira, hususan kuandaa ***Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania***, itakayozinduliwa leo na kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2026 – 2030). Nimefurahi zaidi kuona programu hii itatekelezwa katika pande zote mbili za muungano, kwa kuwa mazingira na rasilimali zake hayatambui mipaka ya kiutawala. Aidha, kwa kutambua kuwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ni mtambuka, naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa wadau wote wa mazingira nchini kuunga mkono jitihada za Serikali katika utekelezaji wa afua zote zilizobainishwa katika programu hii.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi na Wadau wa Mazingira;***
Katika kuhimiza jitihada za kulinda na kutunza mazingira, pamoja na mambo mengine, ningependa kusisitiza kwa Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine, yafuatayo:

(i) Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan Manispaa na Majiji kuazisha Bustani za kijani na kuhakikisha zinatunzwa ipasavyo;
(ii) Mamlaka zinazotoa vibali vya ujenzi kuweka sharti na kusimamia ili kila kibali cha ujenzi kinachotolewa kinaambatana na agizo la kupanda miti isiyopungua mitano (5);

(iii) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kuhakikisha uwepo wa miche ya miti ya kutosha ili kurahisisha na kuwezesha zoezi la upandaji miti nchini;

(iv) Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakala wa Huduma za Misitu kuimarisha udhibiti wa uharibifu wa maeneo yote yanayopandwa miti;

(v) Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia kituo cha Taifa cha kuratibu kaboni kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), kubainisha misitu inayofaa na kuisajili katika biashara ya kaboni;

(vi) Wizara za kisekta kujumuisha fursa za biashara ya kaboni katika mipango, programu na miradi yao hususan fursa zinazoendana na sekta husika;

(vii) Wizara ya ardhi isimamie utekelezaji na uzingatiaji wa mipango, miji na mipango ya matumizi ya ardhi ili kupunguza au kuondoa kabisha changamoto za uharibifu wa mazingira zinatotokana na matumizi ya ardhi yasiyo endelevu;

(viii) Mamlaka za Serikali za Mitaa, kupitia kifungu cha 89 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288, kuimarisha mifumo ya usimamizi wa taka hususan kuanzisha vituo vya kuchakata taka ili kupunguza kiasi cha taka katika madampo na kuchagiza urejelezaji;

(ix) Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Maji kuimarisha usimamizi endelevu wa maeneo ya ardhi oevu; na,

(x) Taasisi za utafiti kufanya tafiti kuhusu mimea/viumbe vamizi ambavyo vinazidi kuongezeka na kuathiri mifugo na mimea mingine katika maeneo mbalimbali nchini.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Wananchi na Wadau wa Mazingira;***

Suala la ulinzi na uhifadhi wa mazingira halina mbadala, kwa kuwa mazingira yetu ndiyo uhai wetu na uchumi wetu. Wito wangu kwa kila mmoja wetu ni kuwajibika kuhakikisha kwamba suala la utunzaji na usafi wa mazingira, ikiwemo udhibiti wa taka linapewa kipaumbele. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kulinda mazingira yetu na kupunguza athari mbaya za mabadiliko ya tabianchi.

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, napenda kutoa shukurani na pongezi kwa wadau wote wa mazingira hususan Mashirika ya Umoja wa Mataifa; Mashirika Yasiyokuwa na Kiserikali; Sekta Binafsi, Vyombo vya habari na Wananchi wote kwa ujumla, kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Serikali katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira kwa ujumla.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natamka rasmi kuwa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka 2026 yamefikia kilele. Sasa nipo tayari kufanya shughuli zilizosalia ikiwa ni pamoja na kuzindua Programu ya Mageuzi ya Kimkakati ya Mazingira Endelevu Tanzania na kutoa Tuzo ya Rais ya Hifadhi ya Mazingira.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza.***